

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**(Kikao cha Thelathini na Moja - Tarehe 22 Julai, 2004)**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa na: -

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2003 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Ngorongoro Conservation Area Authority for the Year ended 30<sup>th</sup> June, 2003*).

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (*TAFIRI*) kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2003 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Fisheries Research Institute for the Year ended 30<sup>th</sup> June, 2003*).

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa na Taasisi ya Utafiti wa Misitu (*TAFORI*) kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2003, (*The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Forestry Research Institute for the Year ended 30<sup>th</sup> June, 2003*).

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

**MHE. SALAMA KHAMIS ISLAM (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 296

### **Barabara ya Kiomboi - Kisiriri - Kidaru**

**MHE. LEONARD M. SHANGO** aliuliza:-

Kwa kuwa Barabara ya Kiomboi - Kisiriri - Kidaru miaka ya nyuma takriban mpaka miaka ya 1970 ilikuwa inapitika kwa magari ya kibiashara hasa malori na mabasi kuwahudumia wananchi wa Bonde la Kidaru na Mto Ndururumo ambao ni maarufu kwa shughuli za kilimo na mazao ya chakula na ya biashara, uvunaji wa mazao ya maliasili na ufugaji na kwa kuwa sasa barabara hiyo imeharibika kabisa kiasi kwamba hata magari madogo kama *Pick Ups* na *Land Rovers* na hata baiskeli haiwezekani kupita pasipo kuhatarisha ajali na upotevu wa maisha ya watu na mali zao na kwa hiyo, kufanya wananchi wa bonde hilo kuwa vigumu kuwa na mawasiliano na Makao Makuu ya Wilaya ya Kiomboi, kupata huduma muhimu za kibiashara, kijamii na kiutawala.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kukarabati na kuifufua barabara hiyo hasa sehemu korofi zaidi?

(b) Je, ukarabati huo utagharimu fedha kiasi gani?

(c) Kwa kuwa ukarabati au ufufuaji wa barabara hiyo unaweza kuwa wa gharama kubwa kupita uwezo wa kifedha, kiufundi na kivifaa wa Halmashauri ya Iramba, je, Serikali haioni kuwa ni busara kuchukua jukumu la kuikarabati barabara hiyo badala ya kuiachia mzigo Halmashauri ya Iramba?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kiomboi - Kisiriri - Kidaru iko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Iramba na ina urefu wa kilometa 25 na sehemu kubwa ni milima. Barabara hii inahitaji matengenezo makubwa ili iweze kupitika kwa vyombo vya usafiri kwa wakati wote. Mvua zinazonyesha mara kwa mara husababisha sehemu kubwa ya udongo wa barabarani kumomonyoka na kuacha mawe mengi yamejitokeza na mengine kuporomoka barabarani kutoka kwenye mwinuko na hivyo kuifanya barabara hii kupitika kwa tabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiifanyia barabara hii matengenezo hasa zile sehemu korofi ili iweze kupitika kulingana na uwezo wa fedha wa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 1995/1996 Serikali ilitumia kiasi cha shilingi 20,000,000/=. Matengenezo hayo yalijumuisha kuondoa mawe barabarani, kuchonga mawe yaliyojitokeza, kuongeza upana wa barabara, kujenga kalvati nne na kujenga barabara kwa kiwango cha zege katika sehemu korofi.

(ii) Chini ya mpango wa Usafiri na Usafirishaji Vijijini (*VTTP*) ambayo ni mafunzo ya matengenezo ya barabara kwa kutumia *labour based technology* yalitolewa mwaka wa fedha wa 1998/1999. Chini ya mpango huu jumla ya shilingi 11,152,000/= zilitumika kuifanyia barabara hii matengenezo kati ya Kiomboi na Kisiriri.

(iii) Katika mwaka wa fedha 2002/2003 Serikali ilitumia shilingi 41,095,320/= kuifanyia matengenezo barabara hii hivyo kufungua baadhi ya maeneo hiyo kwa mawasiliano kati ya Kiomboi na vijiji vya Kisiriri na Kidaru.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kwa mwaka wa fedha 2004/2005 imeomba fedha kiasi cha shilingi 18,490,000/= kwa ajili ya kufanya matengenezo sehemu korofi kati ya Kisiriri na Kidaru.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, fedha nilizozitaja katika sehemu ya (a) ambayo ni nimeunganisha na sehemu (b) ambazo zilitumika kuifanyia barabara hii matengenezo ni fedha za Serikali Kuu zilizotolewa kama fedha za Mfuko wa Barabara au kupitia Mradi wa *VTTP* na hivyo Serikali Kuu haijaiachia mzigo wa kuifanyia barabara hii matengenezo Halmashauri ya Iramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi ambacho kinatengwa kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara inategemea vipaumbele vya Halmashauri husika na hali ya uchumi wa nchi bila kujali barabara ni ya Halmashauri au ya Wizara ya Ujenzi. Hata hivyo, Mheshimiwa Mbunge anashauriwa kuwasiliana na Halmashauri yake ili ichukue hatua zinazohusika kupeleka maombi ya kupandishwa daraja barabara hiyo ili iwe ya Mkoa ambapo itakuwa chini ya Wizara ya Ujenzi. Lakini maombi hayo hayana budi kuelezea umuhimu wa barabara hiyo kiuchumi na kijamii kama rai aliyoieleza katika swali ilikuwa inalenga kufanya utaratibu huo. (*Makofi*)

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Mwaka jana Bodi ya Barabara ya Mkoa, ilikwisha pendekeza kuwa barabara hii majukumu yachukuliwe na Mkoa, je, mpaka sasa ni sababu gani za msingi hatujapewa jibu kuwa barabara hii sasa imekuwa kwa sababu Halmashauri ya Wilaya haina ule uwezo wa kuitengeneza kusudi ianze kupitika na kuwahudumia wananchi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leonard Shango, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yote ambayo yamepelekwa kutoka kwenye Bodi za Barabara za Mkoa bado haziwezi kupata majibu kwa sababu *draft* ya sheria sasa hivi wadau wanaipitia na ndani ya sheria hiyo, ndimo barabara zinatajwa zilizopandishwa na zilizoshushwa. Kwa hiyo, Mikoa yote haijapata majibu ya maombi yao. Itapata majibu ya maombi yao wakati sheria itakapoletwa hapa Bungeni. (*Makofi*)

Na. 297

### **Mapato yatokanayo na Bandari**

**MHE. HADIJA K. KUSAGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Bandari ni moja kati ya vyanzo vikubwa vya mapato kwa nchi nyingi duniani.

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge kwamba ni kiasi gani cha mapato kimepatikana kutokana na kukodishwa/kubinafsishwa kwa bandari?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani za kuboresha Bandari zetu ili kuongeza Pato la Serikali ikiwa ni pamoja na kuboresha maslahi ya wafanyakazi wake?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hadija Kasola Kusaga, Mbunge wa Temeke, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba wa kukodisha Kitengo cha Makontena kwa kampuni binafsi yaani *Tanzania International Container Terminal Services (TICTS)*. Mapato ya Serikali ni ya aina mbili.

(i) Mapato ya pango (*Fixed Rental Income*) ambayo ni Dola za Marekani milioni 3.680 kwa mwaka.

(ii) Mrahaba (*Royalty*) dola za Marekani 13.0 kwa kila kontena likalohudumiwa na *TICTS*.

Hivyo, mapato yaliyopatikana kuanzia Septemba, 2000 hadi 2004 ni jumla ya shilingi bilioni 18.006. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 11.748 zinatokana na kodi ya pango na shilingi bilioni 6.258 ni *royalty*.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ni kuzifanya Bandari za Tanzania kuwa lango kuu la biashara ya Kimataifa kwa nchi zilizoko Mashariki, Kati na Kusini

mwa Afrika, kwa utoaji wa huduma za uhakika, bora, nafuu na zenye faida na maslahi ya kibandari kwa kutumia mbinu na teknolojia ya kisasa pamoja na wafanyakazi wenye ari na moyo wa kufanya kazi. Hatua zifuatazo zimechukuliwa na Serikali kufikia azma hiyo.

(i) Kushirikisha sekta binafsi katika kumiliki na kutoa huduma mbalimbali za kibandari.

(ii) Kuzifanya bandari zote nchini yaani zile za mwambao na za maziwa zimilikiwe na mamlaka moja itakayoundwa (*TPA*).

(iii) Kuwekeza katika miradi ya maendeleo inayowezesha Bandari zetu ziwe za kisasa zaidi na zenye vifa bora vya kisasa na vya kutosha. Aidha, zaidi ya Dola za Marekani milioni 500 zimetumika katika kuboresha miundombinu ya bandari.

(iv) Kuwapatia mafunzo mbalimbali viongozi na wafanyakazi wake ili kuwapatia mbinu mbalimbali za kisasa na kupata uzoefu ambao unawawezesha kutenda kazi zao kwa ufanisi zaidi.

(v) Kuhimiza ushirikiano wa masharika, wadau wanaotoa mchango katika usafirishaji wa mizigo iliyopita bandarini.

(vi) Kutungwa kwa sheria ya kuanzisha maeneo maalum *Export Processing Zones*.

(vii) Kuboresha mawasiliano kati ya Mamlaka ya Bandari na watumiaji wa huduma za bandari kwa kuweka mtandao wa mawasiliano na kompyuta.

(viii) Mwisho kuboresha hali ya ulinzi katika Bandari zetu kwa lengo la kujikinga na vitendo vya kigaidi, uoro wa kutumia meli, dawa za kulevya na biashara haramu.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yenye kuridhisha. Sasa naomba niulize mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Bandari ya Dar es Salaam imekuwa ni ya kwanza katika Afrika kwa kufanya vizuri. Mchango huu umetokana na wafanyakazi wa Bandari lakini bado ipo migogoro mikubwa kwa wafanyakazi kuhusu Serikali na wao wenyewe, je, Serikali inawasaidia nini wafanyakazi hao ili kuweza kutatua migogoro iliyopo na waweze kuendelea kufanya kazi vizuri? (*Makofi*)

(b) Nimewahi kusikia kwamba mizigo inayopitia bandari zetu imepungua kwa kiasi kikubwa sana. Sasa, je, kama usemi huu ni kweli Serikali inatambua ni kwa kiwango gani imepungua na ni kwa nini imepungua? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Khadija Kusaga, kama ifuatavyo:-

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba hakuna migogoro mikubwa ya wafanyakazi bandari, ilikuwepo kwa kupitia Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana, masuala mengi tu ya migogoro hiyo imekamilishwa, labda ijitokeze jana na leo. *(Makofi)*

Pili, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mizigo kwa mujibu wa takwimu tulizonazo haijapungua kwa Bandari ya Dar es Salaam. Katika mwaka 2003/2004 shehena iliyopita pale ni tani 3.19 sawa na asilimia 70.9. Bado Bandari ya Dar es Salaam ni mfano kwa bandari zote za Kusini mwa Afrika. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Bandari ya Tanga ni moja ya Bandari za mwanzo sana katika nchi hii na ambayo ilikuwa inapitisha shehena nyingi sana katika nchi hii na sasa hivi inafanya kazi nzuri ya kupitisha mchango kutoka Bulyanhulu kupeleka Japan na maeneo mengine lakini kwenye hali mbovu sana. Katika mkakati tuliambiwa kuwa upo mkakati wa kuiboresha bandari hiyo na kujenga bandari mpya eneo la Mwambani kwa Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, maeneo yale, je, ni lini mkakati huo utanza ili kuiboresha bandari hiyo na kuongeza uchumi katika nchi yetu hasa katika *Northern Corridor?* *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, kama ifuatavyo:-

Kweli bandari ya Tanga inafanya kazi nzuri sana na kwa mwaka huu hali imeboreka zaidi kuliko ilivyokuwa hapo nyuma. Napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Bandari ya Tanga, imeboreshwa na nina hakika na yeye ni shahidi katika uboreshaji wa huduma hiyo na bado kweli tunayo nia ya kujenga bandari Mwambani kule Tanga, isipokuwa kwanza tunatafuta fedha za kufanya utafiti na hali ya fedha ikiridhisha tutaweza kujenga Bandari ya Tanga, kwa sababu Bandari ya Tanga ina kina kidogo na kule Mwambani kina cha maji ni kikubwa zaidi. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa Bandari ya Lindi ni ya siku nyingi na kwa kuwa Bandari ya Lindi inahudumia Mkoa mkubwa wa Lindi ambao una mazao mengi kama korosho na ufuta na kwa kuwa hata Wilaya za jirani za Masasi na hata Newala, Lindi ni jirani zaidi kwao kuliko Bandari ya Mtwara, je, Serikali lini itaboresha bandari hii ili iweze kuhudumia mizigo ambayo inapitia pale? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dada Maria Watondoha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba Bandari ya Lindi ina umuhimu wa kusafirisha bidhaa ambazo zinatoka Masasi na sehemu nyingine. Lakini nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa bado Bandari ya Lindi, haijatoa uzito unaotosha katika kusafirisha bidhaa. Ni kasma kidogo tu inayopita pale Lindi, labda tuendelee tu kuwashawishi wafanyabiashara wazidishe huduma hiyo ili tuweze kuboresha zaidi na kuhudumia watu zaidi. (*Makofi*)

Na. 298

**Fedha kwa ajili ya Barabara zilizoharibiwa na Mvua za *El - Nino***

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 Serikali ilitenga shilingi 8,602,613,000/= kwa ajili ya barabara zilizoathirika na mvua za *El-Nino (El-Nino Roads Infrastructure)*, mkopo uliotolewa na *ADB* na kwa kuwa miongoni mwa barabara zilizoathirika na mvua za *El-Nino* na mpaka sasa hazijashughulikiwa na zina hali mbaya sana ni pamoja na ile ya Itigi- Rungwa.

Je, ni kiasi gani cha fedha kitatolewa kutoka kwenye fungu hilo kwa ajili ya barabara hiyo ili kufungua mawasiliano kati ya Mkoa wa Singida na Mbeya?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 Wizara yangu ilitenga jumla ya shilingi 8,602,613,000 kutoka mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) kwa ajili ya matengenezo ya barabara zilizoathiriwa na mvua za *El-Nino* Barabara ya Manyoni - Itigi - Rungwa ikiwa ni miongoni mwa barabara hizo. Barabara hiyo ya Manyoni - Itigi - Rungwa imetengewa jumla ya shilingi 450,840,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi umechelewa kuanza kutokana na matatizo yaliyokuwa yamejitokeza huko *Ivory Coast* na kusababisha Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) kuchelewa kutoa kibali cha kuingia mkataba na makandarasi wa kufanya kazi katika barabara zilizoathirika na mvua za *El-Nino*.

Kutokana na kuchelewa kibali, mkandarasi aliyependekezwa kufanya kazi katika barabara za Manyoni - Itigi - Rungwa alijitoa na kusababisha uchambuzi wa kumpata

mkandarasi mwingine wa kufanya kazi hiyo ufanyike upya. Hivi sasa mkandarasi mwingine amechaguliwa na tayari amekwishaanza kazi katika sehemu ya Itigi - Rungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa kwa vipindi mbalimbali matengenezo ya kawaida na yale ya dharura yalikuwa yanaendelea katika barabara hizo ikiwa ni pamoja na ile ya Itigi - Rungwa kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini vile vile naomba nimweleze tu Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba tunatambua na kuthamini kazi nzuri inayofanywa na Wizara yake pamoja na timu yake ya watu wa *TANROADS* Singida. Nawapongeza kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Kwa kuwa kama alivyoeleza katika jibu lake la msingi kwamba matengenezo yaliyohusisha barabara ya kutoka Manyoni- Itigi - Rungwa kilometa 236 lakini mpaka sasa kilometa zitakazoshughulikiwa na hii fedha ya *ADB* ni kilometa 65 kutoka Kilumbi mpaka Rungwa. *TANROAD* Singida wamejitahidi kufanya kazi nzuri kutoka Manyoni mpaka Mgando ambao ni kama kilometa 110. Sasa kwa kuwa kuna kipande kilichobakia cha kilometa 61 ambacho nacho kimeharibika vibaya sana na hizi mvua za *El-Nino* je, Wizara kwa kutumia utaratibu huu wa kuomba mkopo ama kwa kuongeza fedha toka Wizarani itakuwa tayari kufanya namna hiyo ili hii barabara iweze kuwa nzuri zaidi na kazi nyingine nzuri isiharibike? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, kutoka Manyoni Magharibi. Kwanza, nashukuru kwa kuipongeza *TANROAD* na Wizara inatutia moyo. (*Makofi*)

Pili, swali la kuongeza fedha kutoka Wizarani naomba niseme wazi uwezekano wa jambo hilo haupo kwa sababu fedha yenyewe ndiyo hii ambayo tumepanga tayari. Lakini *TANROAD* wataendelea kutengeneza ile barabara ili iwezekane kupitika wakati wote kwa kutumia fedha za *Road Fund Vote*. (*Makofi*)

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na barabara ya Itigi - Rungwa, pia ipo barabara ya Mnazimmoja - Masasi na kwa kuwa shimo la daraja la Nangoo linaua watu kila kukicha lilipohamishwa daraja hilo na *El-Nino*, kwa mfano, juzi watu 13 wamefariki kwa kutumbukia na gari la *Tawaqal*, je, daraja hilo na sehemu ya Chipate itakamilishwa lini ili tupumzike kufa? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Hili ni swali jipya halihusiani kabisa, lakini kama Mheshimiwa Naibu Waziri ana jibu anaweza kutoa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali lisilokuwa na uhusiano sana na swali hili la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, ila ni kwa sababu ni barabara na madaraja basi linahusika na Wizara yangu.



Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata habari juu ya gari lililotumbukia *Nangoo bridge* na tunalijua hili daraja na sehemu ya Chipate vile vile tunajua ubaya wake na tumewaelekeza *TANROAD* waharakishe kutengeneza hivyo, lakini Daraja la Nangoo bado hatujalipatia fedha lenyewe linahitaji fedha nyingi sana.

Na. 299

### **Mafundi wa Barabara - *Technicians***

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA** aliuliza:-

Kwa kuwa Idara ya Ujenzi inayo majukumu makubwa sana katika kujenga na kusimamia ujenzi wa barabara, madaraja na majengo mbalimbali hususan hospitali na madarasa na kwa kuwa sasa kuna ongezeko kubwa la ujenzi wa majengo niliyotaja na kwa kuwa Wilaya ya Mbinga inao *technicians* watatu tu ambao wanapaswa kusimamia shughuli hizo.

(a) Je, *technician* mmoja anapaswa kusimamia barabara ya urefu gani kwa mwaka na madaraja na majengo mangapi?

(b) Kwa kuwa majengo mengi na barabara hazikaguliwi mara kwa mara, je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza watumishi hao muhimu pamoja na kuwapatia nyenzo bora za kufanyia kazi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Idara ya Ujenzi inayo majukumu makubwa sana katika kujenga na kusimamia ujenzi wa barabara, madaraja na majengo mbalimbali. Aidha, ni kweli pia kwamba kuna ongezeko kubwa la ujenzi wa majengo hasa ya shule ya msingi kupitia mradi wa MEM na Hospitali na ongezeko la matengenezo ama ujenzi wa madaraja na barabara toka kuanzishwa kwa mfuko wa barabara. Maongezeko haya yamechangia harakati za utekelezaji wa mpango wa kupunguza umaskini katika jamii kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wabunge wanavyofahamu, jukumu la kuajiri wataalam (*Technicians*) ambao wangesimamia shughuli za ujenzi chini ya Halmashauri ni Halmashauri husika. Wizara ya Ujenzi ina jukumu la kusimamia ujenzi ama matengenezo katika Barabara Kuu, Barabara za Mikoa na Majengo ya Serikali Kuu. Ili Halmashauri zijue ni wataalam (*Technicians*) wangapi na wa aina gani inawahitaji, inatakiwa ijue pamoja na mambo mengine mradi husika ni wa aina na ukubwa gani na mahitaji yake. Ni wazi aina ya miradi na maeneo ilipo itachangia katika kuamua idadi ya vifaa, nyenzo na wataalam.

Aidha, ajira ya watalaam hawa itategemea pia na uwezo wa fedha wa Halmashauri husika, lakini bila kuathiri ubora wa kazi zinazotakiwa kufanywa. Hivyo namshauri Mheshimiwa Mbunge, baada ya kubaini ongezeko la kazi za wajenzi katika Halmashauri za Wilaya, aishauri Halmashauri yake ijipange na kuajiri watalaam husika. Wataalam wazuri wako nchini.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa kutoa majibu mazuri pamoja na kwamba awali swali langu lilikuwa limeelekezwa Wizara ya TAMISEMI. Hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

(a) Kwa kuwa suala la majengo na barabara katika Wilaya kuna barabara zinazosimamiwa na Wizara na kwa kuwa *TANROAD* wanakaa Mikoani kwenye Makao Makuu ya Mikoa na kazi zinafanyika kwenye maeneo ya Wilaya na huku ndiko shughuli za ujenzi zinafanyika, je, Wizara iko tayari kupeleka watalaam wa *TANROADS* wakakae Wilayani ambako ndiyo kuna kazi?

(b) Kutokana na uchache huo wa watalaam, je, Serikali haioni kwamba matumizi yote ya fedha hizo itakuwa ni hasara kubwa hasa ikizingatiwa kwamba wakandarasi wengi huwa wanadanganya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatana na sheria iliyoanzisha *TANROADS*, wao watawajibika na barabara za Taifa yaani Barabara Kuu na za barabara Mkoa. Barabara za Halmashauri zitawajibika na hali ya Halmashauri. Kuwapeleka watu wa *TANROAD* huko kwenye Halmashauri hasa kwamba wapo Mkoani itakuwa ni vigumu sana kwa sababu itabidi kufanya *establishment* mpya ya *TANROAD* na kuongeza mzigo kwa *TANROAD* sasa hivi.

Naomba kwa suala hili, Mheshimiwa Mbunge, akubaliane tu kwamba Halmashauri iwajibike na barabara na majengo husika. Kuhusu uchache wa wataalam wa ujenzi wa majengo na barabara siyo wachache kiasi hicho. Wapo ma-*engineer* wa majengo na ma-*engineer* wa barabara wasiokuwa na kazi wengi sana. Pale Halmashauri yoyote inapokwama kuwapata na kuwahitaji, tunaomba tuwasiliane ili tuwapatie watu hawa, wapo Watanzania hawana kazi. (*Makofi*)

Na. 300

### **Athari za Wakimbizi Wilayani Ngara**

**MHE. GWASSA A. SEBABILI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya 1993/1994 Wilaya ya Ngara ilipokea Wakimbizi zaidi ya 1,000,000 kutoka Rwanda na Burundi na kwa kuwa hali hiyo ilileta athari nyingi Wilayani Ngara kama zile za mauaji, wizi wa mifugo, magari, vyombo vya ndani, mazao mashambani, kuharibu mazingira, Wakimbizi na kadhalika jambo lililoifanya Wilaya hiyo kuingia katika umaskini na kuwakosesha wananchi amani na utulivu wa kuendelea na shughuli zao za maendeleo:-

(a) Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya hasara walizopata wananchi wa Ngara ili Jumuiya ya Kimataifa ifidie hasara hizo?

(b) Je, Serikali inayo mikakati ipi ya makusudi ya kuinua hali ya maisha ya wananchi wa Wilaya ya Ngara ambayo haijapata kutulia hata kidogo tangu mwaka 1948 kutokana na majanga ya Wakimbizi ya mara kwa mara kama yale ya mwaka 1948/1959 hadi 1963, 1993 na 1994?

(c) Je, Serikali inafahamu kuwa Wakimbizi walioingia Wilayani Ngara kuanzia mwaka 1959 hadi 1963 walikuwa zaidi ya 300,000 na kwamba walidumu huko kwa miaka 30 hadi mwaka 1995 na wale wa mwaka 1993 na 1994 ambao idadi yao ilikuwa takriban 1,000,000 wamedumu kwa miaka 10 na hadi sasa 2004 wapo Wakimbizi wa Burundi kiasi cha 100,000 na hivyo Wilaya ya Ngara na Mkoa wa Kagera unahitaji upewe mtazamo wa kipekee na Serikali ili kuinua maendeleo ya wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa historia ya Wilaya ya Ngara inaonyesha imepokea na kuwahifadhi Wakimbizi wengi kwa vipindi tofauti. Wimbi kubwa zaidi ni lile la Wakimbizi waliopokelewa mwaka 1993 na 1994 kutoka Rwanda, jumla yao ilikuwa 500,000 ambao wote walirejea kwao mwishoni mwa mwaka 1996. Kwa takwimu zilizopo mpaka tarehe 30 Aprili, 2004 zinaonyesha kwamba Wilaya ya Ngara ilikuwa na Wakimbizi 73,633 kutoka Burundi. Wakimbizi kutoka Rwanda wote wamerudishwa kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwahifadhi Wakimbizi hao, Wilaya ya Ngara imepata athari mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Athari hizo zimefanyiwa tathmini na Taasisi mbalimbali ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

Baada ya tathmini kubainisha gharama halisi za kupunguza athari za Wakimbizi, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa ilianzisha miradi mbalimbali yenye lengo la kupunguza athari hizo ikiwa ni pamoja na kuendeleza misitu na kupanda miti, kukarabati miundombinu kama barabara na viwanja vya ndege, kukarabati shule na zahanati, kuimarisha usalama kwenye makambi ya wakimbizi na maeneo yanayozunguka makambi hayo kwa kupeleka askari polisi wa ziada na kadhalika. Kwa mfano, kati ya

mwaka 1995 hadi 2002 Shirika la *UNHCR* peke yake lilitumia zaidi ya shilingi bilioni nne katika miradi ya ukarabati wa maeneo yaliyoathirika na wakimbizi Wilayani Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali yenye mwelekeo wa kupunguza athari za wakimbizi. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya Kimataifa inaendelea na jitihada za kusuluhisha migogoro katika nchi za Burundi na Kongo (*DRC*) ili ziweze kupata utulivu na amani. Hali hiyo itawezesha wakimbizi wote warudi katika nchi zao na hivyo kutoa fursa kwa wananchi wa Ngara na maeneo mengine yanayohifadhi wakimbizi kushughulikia maendeleo yao na Serikali na Jumuiya ya Kimataifa itaendelea kuwaunga mkono kwa kutekeleza miradi ya kupunguza athari zilizosababishwa na wakimbizi.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa jibu lake zuri kuhusu athari za wakimbizi Wilayani Ngara. Lakini hata hivyo, naomba uniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wanashirikianaje katika kushughulikia kitu kinachoitwa kinga ya Kibalozi au Kinga ya watumishi wa Kimataifa? Kwa sababu, mwaka 1998 Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya, Musabadu aliyekuwa Afisa Mtendaji wa Kata aligongwa na Mtumishi wa *UNHCR* akafa, leo watoto wake hawasomi, jamaa yake wako katika shida lakini imeshindikana hawa kushitakiwa wala kutoa fidia kwa sababu tu hawa wana kinga ya kibalozi, je, Serikali inafikiria nini kuhusu kitu hicho?

(b) Mwaka huo huo wa 1998 *UNHCR* iliwafukuza watumishi wake 36 wa Kitanzania, *summarily* wanadai shilingi milioni 52, lakini pia wameshindwa kulipwa. Kila wanapodai na suala hili nimelifikisha katika Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, lugha ni kwamba hawawezi kuwalipa na wala hawawezi kupelekwa Mahakamani kwa sababu wao wana kinga ya Kibalozi. Hivi hii ni sahihi kwamba wananchi wa Tanzania wanapata shida kwa sababu ya shughuli za Kimataifa na kwa sababu ya kinga ya Kibalozi basi watu wanaathirika namna hiyo? Serikali inasemaje kuhusu suala hili? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu masuala haya yanahusisha kinga za Kibalozi, kwa hawa waliopata athari na hili Shirika la Kimataifa, namwomba Mheshimiwa Mbunge akubali kwamba Wizara yangu tuwasiliane na tushirikiane na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ili kufanya uchunguzi kuhusu jambo hili tukizingatia kwamba hizo kinga za Kibalozi, lakini kwa sababu watu wetu wameathirika tuone namna ya kuwasaidia. Kwa hiyo, naomba atupatie wasaa tushirikiane na Wizara ya *Foreign Affairs* ili kushughulikia tatizo hili. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bernard Membe, swali la kibalozi, ulikaa Ubalozini.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa kero ya wakimbizi ilizungumzwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania miaka miwili iliyopita alipozungumza na Bunge hili na akatoa changamoto kwamba Jumuiya ya Kimataifa ifanye *review* yaani iangalie mkataba yaani *Refugee Convention* ya mwaka 1959, lakini pia akaeleza kwamba Serikali imechoka sasa kuubeba mzigo huu wa Wakimbizi peke yake yaani *single-handedly* na akaagiza kwamba sasa upo umuhimu wa kulifuatilia suala hili ili wakimbizi wote wanaotoka nchi jirani watengewe eneo kwenye nchi wanayotoka ili Jumuiya ya Kimataifa yaani *United Nation High Commission for Refugee* iwalinde kule kwa sababu fedha zipo, Wizara imetekelezaje changamoto na pendekezo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Rais wetu ametoa changamoto kwamba mikataba hii ya Kimataifa hasa *Geneva Convention* ambayo ilikuwa ya mwaka 1951 ifanyiwe mapitio kwa sababu muda umekwenda na mambo yamebadilika na ni kweli vile vile Rais wetu ametoa pendekezo kwamba hawa Wakimbizi watafutwiwe maeneo salama ndani ya nchi zao wahifadhiwe huko.

Kauli ya Mheshimiwa Rais, Wizara yetu tumeitekeleza kama ifuatavyo:-

Kwanza, tulianza sisi wenyewe kuzungumza na Mataifa mbalimbali ikaona hasa Mataifa makubwa yanasitasita. Kwa hiyo, mwaka 2003 sisi Tanzania tukaitisha Mkutano wa nchi zote, tukakutana nao ili kuweka msimamo wa pamoja, kuwa na sauti moja kuhusu suala hili. Katika Mkutano ule tukaweka msimamo wa pamoja, Septemba, 2003 katika mkutano unaitwa *Executive Committee* ya *UNHCR*, Geneva, nchi zetu hizi kwa sauti moja zikiongozwa na Waziri wetu wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tulipeleka hizi hoja katika Mkutano ule zikaanza kujadiliwa na mjadala bado unaendelea. Kuna baadhi ya nchi hasa wakubwa hawapendi haya mambo, lakini sisi tunaendelea kusukuma jambo hili ili ieleweke na litekelezeke. (*Makofi*)

Na.301

### **Athari za Wakimbizi - Kigoma**

**MHE. FRANK M. MUSSATI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma kwa muda usiopungua miaka 30 umekuwa ukipokea wakimbizi hasa kutoka nchi jirani za Kongo na Burundi na kwa kuwa wakimbizi hao wamesababisha hasara nyingi kwa wakazi wa Mkoa huo ikiwa ni pamoja na ukosefu wa amani, usalama, uharibifu wa mazingira na miundombinu hasa ya barabara:-

(a) Je, Serikali na Jumuiya za Kimataifa inachukua hatua gani za makusudi za kuwafidia wakazi wa Mkoa huo kwa kujitua mhanga kwa niaba ya Tanzania nzima?

(b) Je, Serikali na Jumuiya za Kimataifa au kila moja peke yake itawafuta machozi wakazi wa Kigoma kwa kuwawekea miundominu ya barabara za lami kama ile ya Kigoma - Bukoba - Mwanza na Kigoma - Tabora, pamoja na kuwapelekea umeme wa Gridi ya Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Frank Mussati, Mbunge wa Kasulu Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa muda wa miaka isiyopungua 30 Tanzania kupitia Mkoa wa Kigoma na Mikoa mingine inayopakana na nchi jirani ambazo zimekuwa na migogoro ya ndani imekuwa ikiwapokea na kuwahifadhi Wakimbizi kutoka nchi jirani za Kongo (*DRC*), Burundi, Rwanda na nyinginezo. Kwa kufanya hivyo, Tanzania imekuwa ikitimiza wajibu wake wa Kimataifa unaobainishwa katika Mkataba wa Geneva chini ya Umoja wa Mataifa ambao Tanzania tumeusaini. Ni kweli pia kwamba kuwepo kwa wakimbizi hawa kumesababisha athari mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuzorota kwa hali ya usalama, uharibifu wa mazingira na miundombinu katika maeneo yanayopokea na kuwahifadhi wakimbizi kama Mkoa wa Kigoma. Kwa athari kama hizo, Serikali na Jumuiya ya Kimataifa, hazina utaratibu wa kulipa fidia wananchi wanaoathirika na wimbi la wakimbizi bali hatua huchukuliwa kupunguza athari hizo.

Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali na Jumuiya ya Kimataifa ilianzisha miradi chini ya mpango maalum ujulikanao kama *Special Program on Rehabilitation of Refugee Affected Areas* na miradi mingine chini ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi yaani *UNHCR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi iliyotekelezwa chini ya mipango hiyo Mkoani Kigoma ni pamoja na mradi wa kuhifadhi mazingira kwa kuendeleza misitu na kupanda miti, kukarabati miundombinu kama barabara na viwanja vya ndege, mradi wa ukarabati wa shule za msingi, kuimarisha usalama kwenye maeneo ya makambi ya wakimbizi na maeneo yanayozunguka makambi hayo kwa kupeleka Polisi wa ziada, ukarabati wa zahanati na kadhalika.

Aidha, pamoja na kuwa Mradi huu wa *SPRAA* sasa umefungwa, Serikali inaendelea na jitihada zake za kutafuta wafadhili wengine watakaosaidia kupunguza athari za Wakimbizi na kupunguza umasikini katika Mkoa wa Kigoma. Kwa mfano, hivi sasa katika Mkoa wa Kigoma, umeanzishwa mradi wa kuondoa umaskini unaofadhiliwa na Serikali ya Denmark. Jumla ya shilingi 8,900,000,000/= zitatumika katika mradi huu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina nia ya kuboresha miundombinu na kuhakikisha kuwa umeme na barabara vinasambazwa nchini kote hatua kwa hatua, kadri uwezo wa fedha unavyoruhusu. Serikali inatekeleza azma hiyo kupitia Wizara zinazohusika na masuala hayo. (*Makofi*)

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hali ya Burundi na Kongo zinaendelea kuwa mbaya na wakiondoka wakimbizi kama 1,000 baada ya siku mbili wanaingia wakimbizi 3,000, je, Serikali sasa ina mpango gani wa kujenga makambi mengine katika Mikoa mingine zaidi ya Mkoa wa Kigoma? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati tulionao sasa hivi kusema kweli ni kuwarudisha wakimbizi makwao na sio kusambaza makambi mapya katika Mikoa mingine. Katika jukumu hilo la kuwarudisha makwao, Serikali yetu ikishirikiana na Jumuiya ya Kimataifa, tunafanya juhudi kubwa sana kusuluhisha ile migogoro ili iishe hawa wakimbizi warudi. Kwa hiyo, mwelekeo wa Serikali yetu sasa hivi ni kutengeneza mazingira wakimbizi hawa warudi makwao na sio kutengeneza mazingira ya kujenga makambi mapya ili tuwasambaze katika Mikoa mingine. *(Makofi)*

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja dogo tu.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi katika majibu yake mazuri amesema Serikali ya Denmark imeahidi kutoa bilioni nane kama kuondoa umaskini kwa Mkoa hasa kufuatana na ujio wa wakimbizi, hivi si afadhali hizo shilingi bilioni nane ziunganishwe na bilioni fulani zinazoweza kuchangiwa na Serikali ya Tanzania zikafanya mradi mmoja wa kuhakikisha kwamba tunapata umeme wa Gridi kuliko kusambaza hizo hela sijui kwa watu gani halafu umaskini ukabaki pale pale bila mabadiliko.

Je, hilo haliwezi kusaidia sasa na tukaonana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa ili tukaunganisha tukapata umeme wa Gridi sasa? Je, hilo haliwezekani? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hizi shilingi bilioni 8.9 ambazo zimetolewa na Serikali ya Denmark, katika makubaliano ambayo tumefanya, waliainisha maeneo ambayo Muswada huu uelekezwe. Wameainisha maeneo ya kilimo, maeneo ya huduma ya maji, elimu, hifadhi ya mazingira na miradi midogo midogo ya ku-support miradi midogo midogo ya vikundi vidogo vidogo vya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mfadhili amesema na tumeshakubaliana kwamba fedha hizi zielekezwe katika maeneo haya. Kwa hiyo sasa, kuziondoa katika maeneo haya kuzipeleka kwenye umeme, tutakuwa tunavunja makubaliano ambayo tumeyafanya na Serikali ya Denmark.

Mheshimiwa Naibu spika, kwa hiyo, naomba suala la umeme liendelee na mipango ambayo ilitangazwa na Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

**Vijana Taifa la Kesho**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa upo msemu uliozoeleka na unaotumika sana hapa nchini kwamba vijana ni Taifa la Kesho na kwa kuwa msemu huo huenda kinyume na haki za vijana kwa maana kwamba unawanyima haki yao ya leo na hivyo wasubiri haki hiyo kesho ambayo haipo kwani pale kesho inapofikiwa kuna kesho nyingine tena mbele yake:-

(a) Je, mantiki ya msemu huo iko wapi kwa kuzingatia dunia ya leo?

(b) Je, kuna mantiki gani ya kusema kijana ni Taifa la Kesho na hilo Taifa la kesho ni lipi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa kipindi kirefu vijana wameonekana kuwa ni Taifa la Kesho na msemu huu umechangia kudumaza fikra za vijana katika kuleta maendeleo yao na ya Taifa kwa ujumla kwa kuamini kuwa wao ni Taifa la Kesho na kwamba muda wao haujafika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya mafupi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na mabadiliko mbalimbali ya sayansi na teknolojia yanayoendelea katika dunia ya leo, mantiki ya vijana kuwa Taifa la Kesho inaonekana kupitwa na wakati. Kwa hiyo, vijana hawana budi kuelekeza nguvu zao katika mikakati itakayowaletea mabadiliko na kuwawezesha kupokea majukumu yao hivi leo kama viongozi na nguvukazi ya Taifa. *(Makofi)*

(b) Kama ilivyokwisha jitokeza mantiki ya msemu wa kijana kuwa Taifa la Kesho imepitwa na wakati, hivi sasa vijana wanahamasishwa kuwa ni Taifa la Leo na hivyo basi mikakati yote inalenga katika kuwawezesha ili wajitambue na kujiandaa na kujijengea mazingira mazuri ya kuishi katika dunia ya leo.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.



Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekubaliana nami kwamba msemu huo wa vijana ni Taifa la Kesho umeshapitwa na wakati na vijana ni Taifa la Leo, lakini pia je, atakubaliana nami kwamba vijana wana wajibu wa kuwathamini wazee na kushirikiana nao pamoja na kufuata miongozo yao yenye busara? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa vijana ni nguvukazi ya Taifa hili lakini ndio maskini wakubwa kwa kukosa ajira na mikopo na mambo mengi ambayo yanaweza kuwaendeshea maisha yao, je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuwapatia vijana walio wengi ajira, mikopo na elimu ya biashara hasa huko Vijijini ili kujikwamua kimaisha? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba uhusiano wa vijana na wazee katika kuiongoza nchi hii ni muhimu wakati vijana ni nguvukazi, lakini bila ya busara na hekima ya wazee ni sawa na upepo na tanga bila ya kuwa na nahodha, chombo ni lazima kitakwenda mrama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali lake la pili, Serikali haijaka kimya juu ya kuhamasisha vijana kujiondosa katika hali ya umaskini ndio maana pamoja na Serikali yenyewe kuanzisha mfuko wa maendeleo ya vijana, lakini bado tuko karibu na Wizara ya TAMISEMI kupitia Halmashauri zetu kutenga fungu kwa ajili ya vijana hao hao. Lakini ndio maana Serikali imeamua kusaidia vyuo vya watu binafsi vya ufundi pamoja na VETA ili kuhakikisha tunawapa stadi za maisha vijana waweze kujitegemea. Tunashirikiana vile vile na vitengo vingine vya ndani na nje kama vile UNICEF, FEZ, UNCPA, UMATI, AYA, EMAU, Afya ya Uzazi na Maendeleo ya Mtoto na vyombo vingine kuhakikisha kwamba vijana wanapata stadi zinazohitajika ili waweze kujitea maendeleo yao wenyewe. *(Makofi)*

Na. 303

### **Matatizo Sugu ya Maji kwa Baadhi ya Kata - Kinondoni**

**MHE. PETER KABISA** aliuliza:-

Kwa kuwa miaka ya 1995 hadi 2003 imekuwa miaka migumu sana Jimboni Kinondoni kwa ukosefu wa maji katika Kata zote kumi, lakini kutokana na ushirikiano mzuri na Serikali kupitia Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo maeneo mengi ya Kata hizo kumi sasa yanapata maji safi na salama na kwa kuwa yapo maendeleo machache kama yale ya Kata ya Muzimuni, Mwananyamala, maeneo kati ya Pazi na Mkwajuni na Kata ya Makumbusho, maeneo ya Mchangani na Kisiwani ambayo yamebaki na matatizo sugu ya kukosa maji:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuyashughulikia maeneo hayo ili wananchi wake waweze nao kupata maji safi na salama?

(b) Je, Serikali inatoa agizo gani kwa *City Water Services* ambayo inatoa maji kwa mgao wa wastani wa siku 15 kwa mwezi lakini inatoza viwango vya ujumla vya utumiaji wa maji yaani *flat rate* kwa mwezi mzima?

(c) Je, ni lini *City Water Services* itazifuta bili za maji za wale wateja ambao kwa kipindi kirefu hawapati huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Chini ya mradi unaoendelea wa kuboresha miundombinu ya majisafi na majitaka Jijini Dar es Salaam, jumla ya dola za Kimarekani 164.6 zitatumika katika kukarabati miundombinu ya usambazaji wa huduma za maji safi na uondoaji majitaka. Moja ya kazi zitakazofanyika katika mradi huu ni kuboresha mtandao wa mabomba ya kusambaza maji katika Jiji. Kazi hii inatekelezwa katika awamu nne kati ya mwaka 2004 hadi mwaka 2008. Awamu ya kwanza ya mradi huu itakamilika mapema mwaka ujao na kuondoa matatizo ya maji katika maeneo mengi aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *City Water Services* inatumia utaratibu wa kutoa maji kwa mgao kila baada ya siku moja. Hatua hii imechukuliwa ili kuhakikisha kuwa wakazi wa eneo husika wanapata maji ya kutosha na kwa msukumo au *pressure* inayokidhi siku ya mgao. Uchunguzi uliofanywa na *City Water Services* kwa kipindi cha miezi sita iliyopita imedhihirisha kuwa matumizi ya maji kwa mwezi katika maeneo yanayokuwa yakipata maji kila siku hayajabadilika. Hii inatokana na wakazi wa maeneo husika kuhifadhi maji ya siku ya mgao kwa ajili ya matumizi ya siku inayofuata. Hivyo *flat rate* inayotolewa na *City Water Services* ni kwa ajili ya maji yaliyotoka katika siku hizo 15 ambapo kiwango ni kile kile ambacho kingetolewa katika siku 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana na suala la *flat rate* na kuwa na utaratibu unaoaminika katika kuandaa ankara za maji, jumla ya dira za maji 173,000 zitanunuliwa na kufungwa kwa wateja katika kipindi cha miaka mitatu hadi minne ijayo chini ya mradi unaoendelea kutekelezwa hivi sasa. Kazi hii imeanza mwezi Mei, 2004 na hadi mwisho wa mwezi Juni, 2004 wateja 2,305 walikuwa wameshafungiwa dira za maji.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufuta bili za maji kwa wateja ambao kwa kipindi kirefu walikuwa hawapati maji, Kampuni ya *City Water Services* inaruhusu mteja kwenda katika Ofisi zake na kutaka ufafanuzi kuhusu tatizo la maji. Ikithibitika kwamba mteja alikuwa hapati maji, ankara hiyo inafanyiwa marekebisho ili aweze kulipia kwa kipindi ambacho kimekuwa kikitolewa maji na Kampuni hiyo. *(Makofi)*

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Lakini kama nilivyosema katika swali langu la msingi ni kwamba naendelea kuwapongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya katika Jimbo langu. Sasa ningeomba basi, katika mtandao huu wanaorekebisha sasa hivi, pia

maeneo madogo tu wayarekebishe kwa mfano sehemu za Makanya, Suna, Magomeni Makuti na Kijitonyama ‘A’ na ‘B’ watufikishie maji hayo. Lakini nasema naendelea kuwashukuru kwa kazi nzuri wanayofanya katika Jimbo langu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, *City Water Services* wanafanya ukarabati sasa hivi chini ya mradi na nina hakika maeneo yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja yatakuwa na hali ya nafuu zaidi ifikapo mwaka kesho *phase one* itakapokuwa imekamilika. Kwa hiyo, namwomba awe na subira, nina hakika mambo yatakuwa safi. *(Makofi)*

Na. 304

### **Miradi Ambayo Haikukamilishwa**

**MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza:-

(a) Je, Serikali inatoa maelezo gani kuhusu miradi ya Kitaifa iliyo chini ya Wizara hiyo ambayo imeachwa bila kukamilishwa?

(b) Je, ni miradi mingapi ya umwagiliaji iliyoachwa bila kukamilika na ina thamani gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo miradi mitatu mikubwa ya umwagiliaji maji mashambani iliyoanzishwa kati ya mwaka 1975 na 1989 ambayo haikukamilishwa. Miradi hiyo ni Bugwema ulioko katika Wilaya ya Musoma Vijijini, Mkoani Mara, *Korea Tanzania Agriculture Company (KOTACO)* iliyopo katika Wilaya ya Ulanga, Mkoani Morogoro na Mradi wa Kuendeleza Bonde la Mto Ngono ulioko katika Wilaya ya Bukoba, Mkoani Kagera. Sababu zilizofanya miradi hii isikamilike zinatofautiana kama nitakavyofafanua kwa kila mradi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Bugwema ulianza kujengwa mwaka 1979 na Serikali ya Tanzania na ulikuwa na lengo la kumwagilia maeneo yenye ukubwa wa hekta 1,600 kwa gharama ya shilingi bilioni nane kwa kutumia maji ya kusukumwa kwa *pump* kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi huu ulisimama mwaka 1990 kutokana na usanifu duni uliofanywa na wataalam wa umwagiliaji kutoka Sudan na kutokana na ukosefu wa fedha. Hadi ujenzi uliposimama dola za Kimarekani milioni 1.3 zilikuwa zimetumika kati ya dola za Kimarekani milioni nane zilizokuwa zinahitajika.

Mradi huu ulikabidhiwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa mwaka 1992. Mradi wa Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea na Tanzania (*KOTACO*) uko kwenye Bonde la Mto Rufiji katika Wilaya ya Ulanga na ulianza kujenga tarehe 7 Desemba, 1987 kwa ubia wa hisa sawa kati ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea ikijumuishwa na Kampuni inayojulikana kama *South South Company* na Serikali ya Tanzania ikiwakilishwa na *RUBADA*. Lengo lilikuwa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Kilombero kwa kuanzisha shamba la hekta 5,000 katika eneo la Mngeta.

Utekelezaji wa mradi huu ulisimama mwaka 1993. Hadi wakati huo Serikali ya Tanzania ilikuwa imetumia dola za Kimarekani 11,314,533 na Jamhuri ya Korea ilikuwa imetumia dola za Kimarekani 13,993,892 na mfereji wenye urefu wa kilometa 227 ulikuwa umechimbwa. Ujenzi huu ulisimama kutokana na Korea kuamua kujitoa kwenye ujenzi wa mradi mwaka 1992 na Serikali ya Tanzania kutokuwa na uwezo wa kuendelea na ujenzi. Tarehe 5 Novemba, 1999 *RUBADA* iliingia mkataba na *Kilombero Holding Company* kwa makubaliano kwamba kampuni hiyo ingelipanua shamba kufikia hekta 50,000 kwa mpango wa *BOT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Ngoni lina *scheme* za umwagiliaji wa maji mashambani ya Kakela yenye ukubwa wa hekta 3,000. Nkenge yenye hekta 2,600 na Kajunguti hekta 3,800 katika mwaka 1975 gharama za kuendeleza bonde zima la Mto Ngoni zilikadiriwa kuwa ni shilingi milioni 192,500 katika mwaka huo Serikali ilianza kuendeleza mradi wa majaribio ya Kakashera kwa kuendeleza hekta 32. Mradi huu ulisimama mwaka 1978 kutokana na pampu ya kusukuma maji kuibiwa na kutokana na vita vya Kagera vya mwaka 1978/1979. Aidha, hali mbaya ya uchumi iliyofuata vita iliyofanya Serikali ikose uwezo wa kuendelea na utekelezaji.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mategemeo yetu Kitaifa sasa ili tuondokane na tatizo la upngufu wa chakula na njaa inayotukabili. Ni kwamba kilimo cha umwagiliaji ndiyo hasa tunaelekea kwamba kipewe umuhimu na kipaumbele. Swali ni kwamba, je, Wizara katika maelezo yaliyotoka kwenye jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri, itachukua hatua zipi kutuhakikishia kwamba umwagiliaji sasa unarudishwa na miradi hiyo inakamilishwa ukiwemo hasa mradi wa Mbalika ambao alikuwa ameahidi kwamba utakuwa tayari na utafanya kazi kuanzia mwanzoni mwa mwaka huu ukiwemo pia na mradi wa Mkula maeneo ya Kalemela?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kilimo cha umwagiliaji kinaendelea na tunaitilia mkazo. Kama nilivyowahi kueleza kuwa mwaka wa kwanza tuliweza kufanya hekta kama 5,000, mara ya pili hekta 11,000 na sasa hivi itakuwa zote hekta zaidi ya 23,000. Kwa hiyo, tunaamini na hela zilizotengwa mwaka huu tutaongeza masuala ya umwagiliaji nchini.

Kuhusu Mbarika, suala hili limeshughulikiwa, mradi huu kwanza haukusitishwa, mradi huu ulikamilika lakini baadaye wananchi hawakushughulika nao kikamilifu,

tumeufufua na shughuli zinaendelea. Nimefika mwenyewe kule nina uhakika shughuli zitakuwa bora kuliko ilivyokuwa huko nyuma. *(Makofi)*

Mradi mwingine wa Kalemela ulioambatana na huu ulikuwa kule Wilaya ya Magu ambao unaitwa Nyatwahi. Nimefika, tumetenga hela kwa kutumia fedha za *grinning* kwenye eneo lake. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira tutafika huko anakotaka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafahamu kuna swali moja limebaki. Lakini siwezi kuendelea kuna jambo moja la dharura ambalo ningependa kuwajulisha. Hili swali litatafutiwa nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa masikitiko makubwa ningependa kuwataarifu kwamba mwenzetu, Mheshimiwa Kepteni Theodos James Kasapira, amefariki usiku wa kuamkia leo na Daktari tayari amethibitisha kifo chake.

Kwa hiyo, kutokana na dharura hiyo na kwa sababu sina mwongozo hapa, natamka kwamba kwa hivi sasa nasitisha shughuli za Bunge kwa nusu saa ili tuweze kupata mashauriano na Kamati ya Uongozi ya Bunge. Kwa hiyo, Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi tukutane *Speaker's Lounge* kwa muda wa nusu saa. Kwa hiyo, Bunge litarudia tena ili tuweze kutoa maelekezo yanayofuata, tutarudia tena saa tano kasoro dakika ishirini, Bunge litarudia kwa maelekezo zaidi. Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa tano kasoro dakika ishirini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walianza kulia kwa masikitiko ya msiba uliotokea)*

*(Saa 04.09 asubuhi Bunge lilifungwa kwa muda mpaka saa 04.40 asubuhi)*

*(Saa 04.41 asubuhi Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge baada ya maswali, niliwataarifu msiba mkubwa uliotupa leo asubuhi hii. Nilisema tukutane na Kamati, kwa haraka haraka tumefanya hivyo.

Taarifa ambayo tumepata kutoka kwa utendaji wa Bunge ni kwamba leo asubuhi, kijana wake Marehemu, Mheshimiwa Kepteni Theodos Kasapira, ambaye pia nasikia ndio anamwendesha, alikwenda pale anapokaa kwenda kumchukua. Alipofika pale baada ya kuona hatoki, akaingia ndani akamkuta bado amelala akajaribu kumwamsha lakini hakuamka.

Baadaye yule kijana wake akakimbia kuja kumtaarifu Katibu wa Bunge na kumweleza kwamba: “Nilipokwenda kumchukua baba leo asubuhi nilijaribu kumwamsha hakuamka.”

Baada ya hapo na yeye Katibu wa Bunge akaenda na akafanya jitihada hiyo ya kujaribu kumwamsha, akakuta haamki basi akaenda kumfuata Daktari. Alipofika Daktari baada ya kumpima ndipo akagundua kwamba Mheshimiwa Kepteni Theodos Kasapira, hatuko naye tena. Ndio taarifa zikaja kwetu na ndio pale nikawaarifu na kuwaambia kwamba tutakutana na Kamati ya Uongozi ya Bunge, lakini pia tulikutana na ile Tume yetu ya Bunge, tukafanya majadiliano ya haraka katika maeneo mawili.

Moja, je, katika hali hii, tuendeleo na kazi ya Bunge? Pili, utaratibu wa mazishi na taratibu nyingine zitakwendaje? Lakini pengine kabla sijaendelea, nawaomba sasa tusimame kwa dakika moja kwa heshima ya Marehemu, halafu tutaendelea na matangazo.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walilisimama kwa dakika moja kumkumbuka aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Kuhusu mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ponsiano Nyami, ukae kwanza chini nitoe matangazo, huo Mwongozo utaupataje kabla ya matangazo?

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa naeleza nini tulikuwa tunazungumza.

La kwanza, matatizo haya yalipotokea familia yake imearifiwa hata kabla sijatoa tangazo lile. Kwa hiyo, mke wa marehemu baada ya kupata taarifa hii akasema: “Basi nakuja huko ili niweze kuandamana na mwili wa marehemu mume wangu kwenda nyumbani.” Kwa hiyo, hivi sasa tunafanya utaratibu waweze kuja. Pia kuna watoto wa Marehemu wengine wapo Mwanza na wao wamesema wanakuja na kwa taarifa tuliyonayo ni kwamba watakuja leo kwa ndege wakitokea Mwanza.

Kama nilivyosema kwenye mazungumzo haya kulikuwa na hayo mambo mawili, ya mazishi na je, tuendeleo na shughuli au hapana. La kwanza kuhusu mazishi. Kama ilivyo kawaida hapa ndani, tumeunda Kamati ya kushughulikia jambo hili. Kamati hiyo itakuwa na Waheshimiwa Wabunge wafuatao, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, yeye kwa taarifa tulizonazo ndio Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Morogoro, kwa hiyo, atakuwa kwenye Kamati hiyo pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Morogoro.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ambayo Marehemu alikuwemo, nayo ni Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. William Shija, atakuwa kwenye Kamati hiyo. Pia Katibu wa Wabunge wa Chama chake, Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Juma Suleiman N’hunga, atakuwa kwenye Kamati hiyo.

Pia tutakuwa na Mbunge kutoka Kambi ya Upinzani na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, amemteua *Chief Whip*, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kushiriki kwenye Kamati hiyo. Pia kwa upande wa Wabunge Wanawake, ameteuliwa Mheshimiwa Esha Stima, kuwa kwenye Kamati hiyo. Kama kawaida Kamati

hiyo uratibu wake wote utafanywa na Katibu wa Bunge. Hiyo ndio Kamati ambayo itasimamia masuala yote ya mazishi ya Marehemu Kepteni Theodos Kasapira.

La pili ambalo tumelijadili ni suala la je, tuendeleo na shughuli za Bunge au hapana.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka huu ni msiba wa pili katika Kikao hiki cha Bunge. Tayari tulikuwa na uzoefu huo. Baada ya mashauriano na Mheshimiwa Spika, yeye ameelekeza kwamba kwa hili tayari alishalitolea maamuzi na maelekezo. Mtakumbuka maelekezo ni kwamba msiba ambao utasababisha kusimama kwa shughuli za Bunge ni msiba ambao umetangazwa na Taifa. Hayo ndio maelekezo tuliyonayo kuhusu shughuli za Bunge na kwa sababu hiyo Bunge litaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, hapo ndio mwisho wa matangazo lakini kila mara yanayoendelea, mtakuwa mnataarifiwa. Tuna imani saa kumi na moja tutakapojumuika hapa kwa sababu shughuli za Bunge zinaendelea, mtapewa pia taarifa ya nini kinaendelea kwa sababu mpaka sasa taratibu ya lini mazishi, lini mwili utasafirishwa bado haijawekwa.

Baada ya matangazo hayo, sasa nimpe nafasi Mheshimiwa Ponsiano Nyami, ambaye kwa haraka haraka alitaka maelekezo kabla ya matangazo.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba msamaha, nilidhani labda tuliposimama ndio maelekezo yako yalikuwa yamekwisha, ndio maana nilisema hivyo.

Lakini pamoja na maelekezo yaliyotoka kwa Mheshimiwa Spika, nadhani kama sio leo basi siku zinazokuja, Mbunge kufariki tukiwa katika shughuli...

**WABUNGE FULANI:** Leo! (*Makofi*)

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika,...

**WABUNGE FULANI:** Hiyo Wizara imepita.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge amefariki wakati Bunge linaendelea tena amefariki katika mji na kwa hiyo, naweza kusema katika viwanja vya Bunge linaloendelea na maiti yake ipo katika eneo hilo hilo ambapo Bunge linaendelea, halafu ninyi mnaendelea eti tu kwa sababu mpaka Taifa litangaze kwa utaratibu.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna!

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mimi nilikuwa naona mantiki pengine kama Mbunge huyo angefia mbali na eneo ambapo Bunge linafanyika, pengine sura ingekuwa tofauti lakini wakati huu Bunge linapoendelea, maiti ipo hapa hapa na sisi tunaendelea na

Bunge, hivi huo ni uungwana, huo ni utu? Je, tatizo hasa ni lipi, muda au suala la uchumi? (*Makofi*)

Mimi naomba nipate maelekezo na hiyo sababu ya kusema mpaka itangazwe Kitaifa wakati maiti iko hapa siiafiki na kwa kweli sio ubinadamu na wala sio nzuri na nadhani Wabunge ndio wangeweza kuamua sasa kwamba tunabadilisha kanuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi sijui mna-*support* nini kwa sababu hajatoa hoja alikuwa ...

**WABUNGE FULANI:** Ametoa!

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Nimesema kwamba natoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Taratibu, taratibu kabisa, hapa pana Naibu Spika anaongoza kikao hiki, tutakwenda kwa utaratibu wa kanuni zilivyo wala msiwe na wasiwasi.

Waheshimiwa Wabunge, wakati msiba wa mwenzetu Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, ulipotokea baada ya kumaliza msiba ule, Mheshimiwa Ponsiano Nyami sijui kama wakati ule ulikuwepo, lakini Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, alisimama akasema hayo hayo ambayo umeyasema. Wakati ule mimi nilikuwa hapa nikasema kwa Kanuni nilizonazo hazinipi mwongozo wa namna ya kulishughulikia jambo lenyewe. Lakini nikamwambia Mheshimiwa Abdillahi Namkulala na Waheshimiwa Wabunge kwamba nitalifikisha kwenye uongozi wa Bunge na vikao rasmi. Nikafanya hivyo, siku iliyofuatia.

Jumatatu Mheshimiwa Spika, alitoa mwongozo na maelekezo yake kuhusu jambo hili. Sasa kwa mujibu wa Kanuni nilizonazo kwamba Mheshimiwa Spika, anayo mamlaka ya kuweka kanuni pale ambapo anaona uendeshaji bora wa shughuli unafanywa.

**WABUNGE FULANI:** Ahaaa!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, ninyi mmefiwa na mimi nimefiwa.

**WABUNGE FULANI:** Eeeh, sawa.

**NAIBU SPIKA:** Na nataka kuwaarifu kwamba Mheshimiwa Kepteni Theodos Kasapira, amekaa Tunduru miaka kumi kama *DC*, namfahamu, imenigusa. Kwa hiyo, naomba sana tusikilizane nini tunachosema na hiki ni chombo cha Bunge.



Mimi ninachoweza kusema kwa maelekezo ambayo yapo katika shughuli za Bunge na sikuishia hapo nimeongea na Spika mwenyewe na akasema yeye tayari ameweka taratibu ya kushughulikia jambo hili.

**WABUNGE FULANI:** Ahaaa, hiyo leo hapana.

**NAIBU SPIKA:** Huo ndio Mwongozo wangu kama alivyotaka Mwongozo Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

Mwongozo wa Spika, ninyi mnaunga mkono au Mwongozo wa Spika?

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Kuna hoja.

**NAIBU SPIKA:** Hebu tumpatie Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ambaye ana silaha ya kanuni mkononi.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kwa huzuni kabisa niseme kwamba, namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie Kanuni ya 38 ya Kanuni zetu za Bunge, Toleo la mwaka 2004, inasema kama kuna jambo la dharura na muhimu kwa umma, Mbunge anaweza kuomba Bunge lisimame. *(Makofi)*

Mimi ninaamini kabisa kwamba kifo cha Mbunge aliyefariki wakati Kikao cha Bunge kinaendelea, ni jambo la dharura na ni jambo linalogusa umma, kwanza kwetu sisi kama Wabunge na linalogusa umma kwa Watanzania waliomchagua na Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utanikubalia niendeleo, naomba sasa nitoe maelezo kidogo kwamba kutokana na dharura hii ni jambo la ajabu na la kusikitisha kwamba sisi Wabunge ambao ni familia moja. Tunapata msiba mkubwa namna hii na Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kepteni Theodos Kasapira, tulikuwa naye jana jioni. Tumefanya naye kazi mpaka saa mbili kasoro robo usiku tulipoondoka hapa. Leo, sasa hivi hayupo. Ni jambo la ajabu kwanza kutegemea kwamba sisi tutaendelea na kazi ya Bunge ya kuchangia wakati tuna huzuni kubwa. Ni kinyume cha utamaduni wa Mtanzania, msiba unatokea ndani ya familia, familia inaendelea na kazi kana kwamba hakuna kilichotokea. *(Makofi)*

Naomba radhi kwamba nimejisikia kwa sababu jana Mheshimiwa Kepteni Theodos Kasapira, tulikuwa tunawasiliana wakati tuko ndani ya kikao hapa kama ilivyo kawaida yetu Wabunge tuna *messages*. Kwa hiyo, suala hili linamuuma kila Mbunge kiasi kwamba hata leo kuongea inakuwa ngumu. *(Makofi)*

Naomba kutoa hoja sasa kwamba kutokana na dharura hii na kwa kutumia kifungu hiki, Bunge lisimame siku ya leo na mwongozo uliotolewa na Mheshimiwa Spika, utenguliwe na Wabunge kwa kuwa ndio wenye maamuzi ya mwisho katika masuala yoyote mazito. *(Makofi)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Na watu wanatoka nje!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa nampa nafasi AG kama ana lolote la kusema kabla sijawahoji.

**WABUNGE FULANI:** Ahaaaaa!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwa huzuni na masikitiko makubwa, napenda niungane na wananchi, wapigakura wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kupotelewa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Kepteni Theodos Kasapira. Tunaomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kanuni zetu, kama ulivyotuongoza ni sahihi kabisa, hoja hii kwa mujibu huo lakini kwa kanuni hiyo hiyo, fasili ya nne, uamuzi huu ni wa kwako wewe mwenyewe, utapima kama utaona suala hili ni la dharura, halisi na muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa hali tunavyoiona kwa sababu wote tumeguswa sana na suala hili, mimi katika kuchangia kama watakavyochangia Waheshimiwa Wabunge wengine, naona suala hili limetugusa sana, ni vizuri tukaahirisha shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa natoa ushauri tuahirishe mpaka saa kumi na moja jioni.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hatujui kama ulivyotuelezea sasa hivi, utaratibu wa mazishi utakuwaje. Tutoe fursa hiyo kwa familia kufika hapa Dodoma, tuweze kuwafariji na tushauriane kwa utulivu lakini kwa kutambua pia kwamba tuna majukumu ambayo tumetumwa na wananchi kuja kuyafanya.

**WABUNGE FULANI:** Ndio, ahaaa!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi huo ndio ushauri wangu, nakushukuru sana.

**WABUNGE FULANI:** Ahaaaa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunayo hoja iko mbele yetu ambayo ameitoa Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ambayo inasema...

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Ponsiano Nyami!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, hakutoa hoja, aliomba Mwongozo wa Spika, aliyetoa hoja halisi ni Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa. Sasa nini hoja yake? Amesimama hapa akachukua Kanuni ambayo inasema: “Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yeyote aweza kutoa hoja kuwa Bunge liahirisha shughuli zake kama zilivyoonyeshwa katika Orodha ya Shughuli ili lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.” Ndio hoja ambayo ameitoa.

Kwa hiyo, hoja yake wakati nitakapowahoji ni kuahirisha shughuli zile na kujadili shughuli nyingine. Kwa hiyo, naomba hapo tuelewane tu, mtulie ili twende kwenye *process* hiyo vizuri iweze kutuvusha sawasawa.

**WABUNGE FULANI:** Sawasawa.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, nitawahoji juu ya hoja ya kuahirisha shughuli sio Bunge, kuahirisha shughuli ili tujadili jambo hilo la dharura na hapo ndani sasa kama kuna mtu mwenye hoja anaweza kutoa hiyo hoja yake, tumeelewana?

**WABUNGE FULANI:** Ndio.

**NAIBU SPIKA:** Sawasawa. Sasa hoja aliyotoa Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa ya kusimamisha mjadala uliokuwa unaendelea ili tuzungumzie suala muhimu, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, shughuli zile za Bajeti tulizokuwa tunaendelea nazo tumezisimamisha ili tujadili hili ambalo ni muhimu na kweli wote limetugusa, tunaona ni muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nani angependa kuchangia? Nampa nafasi Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, ambaye alitoa hoja wakati ule, aweze kuzungumza.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa masikitiko makubwa, nisingependa kuzungumza mengi ila tu mchango wangu ni kwamba naomba kutoa hoja Bunge hili lisitishwe kwa ajili ya dharura hii mpaka kesho asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imetolewa ...

**WABUNGE FULANI:** Na imeungwa mkono.

**NAIBU SPIKA:** Imeungwa mkono, sawa.

**WABUNGE FULANI:** Kujadili.

**NAIBU SPIKA:** Kujadili?

**WABUNGE FULANI:** Ndio.

**NAIBU SPIKA:** Taratibu. Hapa kuna Kanuni, mimi nafuata Kanuni. Tumeahirisha shughuli zilizokuwa zinaendelea ili kujadili.

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, imetolewa hoja sasa tunajadili.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nijadili hoja hii. Kwa masikitiko makubwa. Niungane na wenzangu waliotangulia kutoa hoja hii kwamba, tuahirishe Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba juzi tulifiwa, tukasema kwamba hii ni mara ya kwanza na Waheshimiwa Wabunge tukaagiza kwamba kama kulikuwa hakuna utaratibu wa kuweza kuahirisha Bunge sasa ni muda muafaka ili viongozi wetu mkakae muweze kutuandalia utaratibu ambao utatusaidia tuwe tunautumia pindi tunapofariki humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha ni kwamba, tumechelewa kufanya hilo mpaka tunakutwa na lingine, sasa tunaendelea kufa huku tunaendelea kuchangia. Kwa hiyo, imekuwa kama vile tuko vitani kwa maana tunapigana, akifa mwenzetu tunamrudisha nyuma sisi tunasonga mbele na vita.

Kwa hiyo, mimi naunga mkono kwamba wakati mnaandaa utaratibu na kwa kweli tunaomba mfanye haraka, leo tuahirishe mpaka siku ya Jumatatu ili tuweze kuja kuendelea na Bunge hili, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ningependa pia kuwakumbusha kwamba Kanuni zetu zinasema mjadala huu utakuwa wa nusu saa.

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Napenda niungane na wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kuombeleza nao katika msiba huu mkubwa ambao umewapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipoangalia tena tutakuwa tu kwenye *session* mpaka jioni. Mimi sidhani kama suala hili linahitaji mjadala mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ametusaidia sana kwa kutuelekeza kwenye kifungu ambacho tunaweza kukitumia ili kufikia uamuzi wa suala hili. Baada ya maelezo aliyotoa Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, *Attorney General*, Mheshimiwa Andrew Chenge, ametoa maelezo mazuri tu na kutoa hoja na hoja yake ilikuwa ni kwamba Bunge liahirishwe mpaka jioni saa kumi na moja. Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, ametoa hoja tofauti na *AG* na yeye hoja yake ni kwamba Bunge liahirishwe mpaka kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nafikiri kilichobaki hapa ni uamuzi wa Bunge kwamba tunachukua hoja ipi ya *Attorney General* au ya Mheshimiwa Abdillahi Namkulala na pia kuna hoja ya tatu ya mpaka Jumatatu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa William Kusila, hoja iliyopo ni moja tu, *Attorney General*, Mheshimiwa Andrew Chenge, naye alikuwa anachangia, hakutoa hoja. Maana lazima ujue katika mchango au mapendekezo kuna kitu kinaitwa hoja. Sasa hoja iliyopo mbele yetu ambayo itajadiliwa kwa muda usiozidi nusu saa ni ya Mheshimiwa Abdillahi Namkulala. Ndiyo hiyo najaribu kutoa nafasi ya mtu yeyote kuchangia na si vyema kuzuia majadiliano hayo maana ni hoja inayojadiliwa kwa nusu saa. Kwa hiyo, ningependa uachie tu tujadili.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee basi.

**NAIBU SPIKA:** Sawa, endelea.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hoja yenyewe haihitaji mjadala au maelezo marefu kwa sababu ya umuhimu wake unaeleweka, naomba basi niunge mkono hoja ya kuahirisha kikao hiki mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie. Kwanza, mimi naunga mkono hoja kwamba Bunge liahirishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Bunge la Tanzania linaundwa na Wabunge na Wabunge tulishasema hii Kanuni ifanyiwe kazi mara moja kwa sababu hatujui leo mwenzetu katangulia, kesho Msindai atafuata au mtu mwingine. Kwa hiyo, wakati Bunge linaahirishwa na Kikao cha Kamati husika kikae ili kuendelea kujadili juu ya kurekebisha hiyo Kanuni ili Mbunge anapopatwa na tatizo tufanyeje, tusingoje mpaka msiba wa Kitaifa kwani na sisi ni Taifa humu ndani. Ni lazima tuwe na maamuzi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nawaunga mkono wale wanaosema Bunge liahirishwe.

**WABUNGE FULANI:** Mpaka lini?

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mpaka baada ya mazishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yangu ni kwamba, mpaka maiti iondoke Dodoma ndio shughuli za Bunge zianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda tena niwaelekeze kuhusu utaratibu, hoja iliyopo mbele yetu ni ya Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, ambaye ametoa hoja kwamba, Bunge liahirishwe mpaka kesho saa tatu asubuhi na ndio tunayoijadili.

Karibu Mheshimiwa William Lukuvi, *Chief Whip*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nianze kwa kutoa pole nyingi sana kwa familia ya Marehemu, kwa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Morogoro na Waheshimiwa Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke peponi roho ya Marehemu Kepteni Theodos Kasapira, *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyopo mbele yetu ni ya Mheshimiwa Abdillahi Namkulala na mimi nimesimama hapa sitaki kupoteza muda bali nimesimama kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Abdillahi Namkulala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuunganisha na maelekezo uliyoyatoa na umuhimu wa jambo lenyewe, naafiki kabisa maelezo ya Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, kwamba ingefaa leo na hasa kwa sababu tunazingatia Mama mfiwa anakuja

na watoto wake kama ulivyosema wamekodi ndege wanakuja, kwa vyovyote vile leo itakuwa ni shughuli kubwa ya maandalizi haya na sisi tutahitaji kushiriki hapa na pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, kwamba Bunge liahirishwe leo mpaka kesho asubuhi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kuna mtu mwingine tena?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa kufuata utaratibu.

Sasa hoja iliyopo mbele yetu ni ya Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, aliyetoa hoja kwamba kutokana na msiba mkubwa na simanzi iliyotupata Waheshimiwa Wabunge kwa leo tuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kusitisha shughuli za Bunge kwa ajili ya shughuli za maandalizi ya mazishi  
ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Kutokana na azimio na hoja hiyo kukubaliwa na Bunge hili, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.19 asubuhi Bunge liahirishwa mpaka siku ya Ijumaa  
tarehe 23 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*